# viazi

agari hayo yakikwa-
nika kuwaajiri vijana
usombelea magunia
ha ili mzigo upun-
kishalikwamua gari
a kupakia na hivyo
a kubwa.
ni, Katibu Mkuu wa
jenzi, Uchukuzi na
(anayeshughulikia
Mwakalinga, alim-
ja wa Wakala wa
ni (Tanroads) Mkoa
azary Rwekaza, kui-
genezo ya dharura
. Alisema itengene-
go cha changarawe
kilomita 90 ili wa-
itumia waendelee
na bora ya usafiri
a maeneo mengine.



CM) wa Mkoa
dani katika eneo

# jibu

eleo zenye kuku-

a ya Mshewe, Es-
ma yeye ni mion-
vake waliopigwa
ombea nafasi ya
2015, alisema li-
kejeli alisimamia
eleo na hatimaye
pinzani ambaye
aume.
a kuadhimisha
e Dunia, lazima
ya kuhakikisha
ji wanajitokeza
uzi katika nafasi
ia udiwani hadi

# Wapewa zigo udhibiti mifugo mashambani

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

VIONGOZI wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wametakiwa kuhakikisha mifugo haingii kwenye mashamba ya mipunga ambayo yamelimwa ili kuepuka migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mtendaji wa Mamlaka ya Mji wa Rujewa, Tuntufye Chamba, wakati akizungumza na wenyeviti wa mitaa wa mamlaka hiyo, alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wakulima kuwa wafugaji wanaingiza mifugo kwenye mashamba yao.

Alisema wafugaji wanaotajwa kuingiza mifugo kwenye mashamba wanatumia kisingizio cha kufuata majani ya malisho ambayo yako kando kando ya mashamba ya mpunga, lakini kutokana na usimamizi mbovu wa wafugaji hao ng'ombe huvamia mashamba na kutafuta mazao.

Aidha, mtendaji huyo alisema katika kipindi hiki cha msimu wa kilimo ni vyema mifugo ikazuiliwa kuingizwa kwenye mashamba yote mpaka pale shughuli za kupanda hadi kuvuna mpunga zitakapomalizika na kama ni kuruhusu mifugo basi iwe ni ridhaa ya wakulima wote.

"Hatutaki migogoro kwenye mji wetu baadhi ya sehemu tuna wafugaji na kwingine kuna shughuli za kilimo hasa mpunga, pande hizi mbili lazima tuzisimamie ili tusiingie kwenye migogoro," alisema Chamba.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji huo, Chameta Godigodi, alikiri kuwapo kwa malalamiko ya baadhi ya wenyeviti kutumia madaraka yao kuruhusu mifugo kuingizwa kwenye mashamba yanayolimwa.

Aliwataka wenyeviti kuwa na msimamo katika kutekeleza majukumu yao, huku wakiweka usawa kwenye maamuzi ili kuepuka migogoro itokanayo na mwingiliano usiofuata utaratibu.

Baadhi ya wenyeviti wa mitaa wa mji huo, walisema wapo baadhi ambao wamekuwa wakiendekeza rushwa ya kupokea fedha kutoka kwa wafugaji ili kuruhusu mifugo itafune mazao bila kuchukuliwa hatua.

Scanned by CamScanner

kupitia
Pemba.
imbo
eiman
o taarifa
Wesha
i ya
ulevya
ema
nika zaidi
kwamba
ubuti wa

akiingiz-
Pemba
na
jirani
a eneo
heweni.
Kilimo,
Uvuvi,
alisema
nia
va na
fanya
va
Unguja

...ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar, Mustafa Aboud Jumbe akizungumza wakati akifunga kikao kazi cha ushirikiano kwenye sekta ya ujenzi baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kilichofanyika kisiwani Pemba jana. (Na Mpigapicha Wetu)

# *Ufungaji na ufunguaji wa pweza wanufaisha wavuvi*


UONGOZI wa Kamati ya Uvuvi ya Kijiji cha Mtende Mkoa wa Kusini Unguja umesema wavuvi wa pweza wameanza kufaidika na utaratibu wa ufungaji na ufunguaji wa uvuvi wa samaki hao kwa zaidi ya miezi mitatu kwa lengo la kutoa nafasi ya ukuaji na kupata mavuno mazuri.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Uvuvi wa pweza ya kijiji cha Mtende, Shaaban Sijamini Khatib alisema hayo wakati alipokutana na waandishi wa habari waliotembelea kamati hiyo na kuona kazi wanazozifanya.

Utaratibu wa ufungaji na ufunguaji wa uvuvi wa pwenza ulianza mwaka 2017 kwa lengo la kuwawezesha wavuvi kupata mavuno mengi zaidi baada ya kuzuia uvuvi huo kwa zaidi ya miezi mitatu na kutoa nafasi kwa ukuaji wa pweza.

Alisema katika awamu ya kwanza walipoamua kuanza utaratibu wa kufunga na kufungua uvuvi wa pweza, wakati wa mavuno yake walipata Sh milioni 1.5.

Alisema hizo ni fedha zilizoingia katika mfuko wa Kamati ya uvuvi zinazotokana na makato ya Sh 1,000 kwa kila mvuvi anayevua pweza baada ya kuruhusiwa kuanza uvunaji baada ya miezi mitatu.



"Faida ya ufungaji na ufunguwaji wa pweza baada ya kuzuia uvuvi wake katika kipindi cha miezi mitatu tumeiona, wapo wavuvi hujipatia Sh 180,000 kwa siku baada ya kuvua pweza zaidi ya kilo 30," alisema.

Mmoja wa mjumbe wa kamati hiyo ambaye pia ni mvuvi wa pweza, Hidaya Mohamed alisema miongoni mwa wavuvi wanaonufaika na uvuvi wa pweza katika utaratibu wa kufunga na kufungua katika kipindi cha miezi mitatu ni wanawake.

"Wakati wa uvunaji wa pweza, wapo wanawake wengi wanaokwenda baharini na kushiriki katika zoezi la kuvua samaki na kujipatia fedha," alisema.

Ufungaji na ufunguaji wa pweza ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa Swiofish unaotekelezwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi kupata mapato mengi na kulinda mazingira ya baharini na uvuvi haramu.

Mkuu wa doria za uvuvi katika mradi wa Swiofish, Haji Shomari alisema wamejipanga vizuri kuona uvuvi haramu unadhibitiwa na hauna nafasi katika mradi unaotekelezwa wa Swiofish.

Alisema wanafanya doria katika nyakati tofauti kwa ajili ya kuwabaini wavuvi ambao wanafanya shughuli za uvuvi lakini hawana leseni halali za kazi hiyo.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inatekeleza mradi wa uboreshaji na usimamizi wa utawala wa uvuvi katika nchi za ukanda wa bahari ya kusini unaojulikana kwa jina la Swiofish kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia ambapo uvuvi wa samaki wa miambani pamoja na pweza umepewa kipaumbele.

Scanned by CamScanner

nyama, ote wa kujadili emsha

2 kulingana na ukubwa, na kupanda bei ni kutokana na makubaliano na mlaji na mfanyabiashara, kwani ni soko huria," alisema Magige.

HA WETU



i- udi

va

patiwa wilaya kiny-

a ush- isaidia no vya mu ya ashara, asaidia wama katika miezi shirika

, Hap- alipata hizo a wa- Idara ada ya ii toka

# TBS yafunga machinjio

**Na NATHANIEL LIMU -SINGIDA**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limefunga machinjio ya Manispaa ya Singida kwa muda usiofahamika kutokana na kasoro na upungufu mkubwa.

Hali hiyo imesababishwa na kukukithiri kwa uchafu ambao ni hatarishi kwa afya za binadamu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, baada ya kukagua machinjio hayo, Ofisa Usalama wa Chakula Kanda ya Kati, Vicent Mateo alisema muda mrefu wamepokea malalamiko mengi kuhusu machinjio hayo.

Alisema malalamiko hayo, yalitolewa na baadhi ya wakazi jirani.

"Malalamiko haya ni pamoja na machinjio kutiririsha maji machafu yaliyochanganyikana na damu.

"Maji hayo ambayo yanapita maeneo ya makazi ya watu, yana harufu mbaya ambayo haivumiliki," alisema Mateo.

Alisema wamebaini mfumo wa maji ni mbovu, pia ujenzi wa mfereji wa maji machafu, kuelekezwa kwenye makazi ya watu.

"Kasoro nyingine ambayo ni mbaya zaidi ni jengo la shimo la kutupia mizoga.

"Jengo lenyewe ni chakavu kupindukia. Harufu mbaya inayotoka kwenye shimo hilo inawakosesha amani watu wanaoishi jirani. Kwa ujumla mazingira ya machinjio hayo ni hataridhishi," alisema Mateo.

Alisema machinjio hayo yatafunguliwa pindi maelekezo yote yatakapofanyiwa kazi.

Ofisa Usalama wa Chakula, Maua Saidi, alisema yapo maradhi ya mnyama au mifugo yanaweza kuambukiza binadamu.

"Maradhi hayo ni pamoja na TB (kifua kikuu).

"Shimo hili la kutupia mizoga, kutokana na ubovu wake linaweza kuchangia maradhi kwa watu wanaoishi jirani," alisema Maua.

Scanned by CamScanner